

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
16 Agosti 2008**

Waliohudhuria

Ally Athuman Jumbe
Ally Saidi Mwishehe
Ally Salum
Amar Shanghavi
Aseli Wilison
Bashiri Rashidi
Beda John Mkusu
Dominata Rwechungura
Edgar R Paulo
Elaine Baker
Frank Peter Rwechungura
George Kabogo
Husein Hamza Hamisi
Hussein Idda Mkopi
Juma Ali Salehe Jongo
Juma Hassan Chibaya
Juma Imori Rugole
Kibwana Mohammad Msiga
Nickson Kilunga
Paulo Atibu Hatibu
Pendo January
Ramadhani Rajabu Nyengo
Shukuru Hassan
Sosthenes C Amlima

Ofisi

Mafundi wa Mejah walipaka rangi ya nembo ya UWABA ofisini na picha za baisikeli za aina mbali mbali kwenye mlango. Bado watapaka rangi ya jina la UWABA nje ya ofisi. Juma alinunua rangi Tsh 2,500.

Shukuru alinunua bao nyeusi ya 4.5 feet x 4 feet kwa Tsh 25,000 – alitumia Tsh 21,000 ya hela ya UWABA aliyopewa wiki jana na Tsh 4,000 kutoka hela ya UWABA ya Juma. Pia alichangia hela yake Tsh 2,000 kwa usafiri na alichangia chalk.

Mradi wa Usalama barabarani - Wamba Memorial Fund na video ya kufundisha
Elaine aliwasiliana na Bwana Wamba wa Chuo cha Usafirishaji kuhusu kutumia uwanja na alisema tuandike barua. Aliandika na Juma atamletea jumatatu.

Tulikubaliana kutana ofisini saa tatu wiki ijayo na kwenda Mabibo pamoja kutengeneza video.

Paulo alipendekeza tuweke taarifa kuhusu UWABA na malengo yetu ndani ya video. Ally Athman alipendekeza tuweke faidha za baiskeli na tuombe dereva wa magari kuheshimu wapanda baiskeli. Shukuru ataongea kuhusu wapi kuendesha barabarani na kuwa makini. Upendo ataongea kuhusu alama za mkono. Wanachama watamkumbusha Mussa Alex aje kwa sababu yeye ni mfano wa mtoto wa shule anayeenda shuleni na baiskeli. Ally Saidi Mwishehe atasafirisha bao nyeusi mpaka Mabibo kwa guta.

Mkutano wa kila mwezi

Elaine aliandika barua kuwaalika TANROADS, halmashauri la jiji na traffic police kwenye mkutano wa UWABA tarehe 30 Agosti. Tuliongea kuhusu kuwakaribisha chakula wakija. Tulikubaliana washiriki katika mkutano wapate bites na soda kutoka hela za UWABA ambayo itaweza kuwa na gharama ya Tsh 25,000 na Edgar atafanya utafiti zaidi.

Rais Kikwete

Elaine aliweka masahihisho ndani ya barua na Juma atapeleka wiki hii.

Msafara wa Baiskeli

Wakati wa wiki Juma alipeleka barua kwa Ubalozzi wa Uholonzi, Ubalozzi wa Ireland na Kampuni ya Guta. Elaine alipokea jibu kwa email kutoka ubalozzi wa uholonzi kwamba mtu atakayeshughulika maombi yetu atarudi mwisho wa agosti na tutapata jibu wakati ule.

Elaine aliandika barua kwa Bakhresa, Ultimate Security na National Microfinance Bank na Juma atazipeleka wiki hii. Atatumia barua kwa vodacom kwa Amar ambaye atapeleka kwa vodacom.

Amar alisema kuna duka makutano ya mitaa ya Morogoro Road na Indira Ghandi Street ambapo tutaweza kupata baiskeli ambazo zina gia kwa Tsh 80,000 kama tunanunua zaidi ya moja mara moja.

Vipeperushi

Wakati wa wiki Paulo, Aseli na Shukuru walisahihisha sehemu ya ofisi kwenye vipeperushi. Wanachama wengine walichukua chache kusambaza lakini nyingi tunazihifadhi mpaka matukio yetu.

Kibwana

Husein Hamisi alitoa repoti kwamba kurekebisha baiskeli ya mkono ya Kibwana itakuwa Tsh 13,500 kwa vifaa vya breki, Tsh 7,500 kwa tubu, Tsh 15,000 kwa tairi na Tsh 2,000 kwa sehemu ya pedali, jumla ni Tsh 38,000, na tuweke Tsh 1,000 ya ziada kwa vitu vidogo vidogo. Wanachama walikubali kutumia hela kiasi hii ya UWABA kurekebisha baisikeli ya Kibwana.

Mambo ya hela

Juma alitumia Tsh 4,000 kwa bao nyeusi, Tsh 2,500 kwa rangi ofisini, Tsh 1,500 ya photocopy, Tsh 300 kurekebisha pancha kwenye baiskeli yake ya kazi ya UWABA, Tsh

200 kwa bahasha na Tsh 500 kwa hela ya simu. Anabaki na Tsh 29,150 ya hela ya UWABA.

Ally Saidi Mwishehe hajaleta hela ya guta – ataleta wiki ijayo.

Mambo mengine

Tulifungua faili kwa ajili ya makala ya magazeti ofisini.

Guta moja ya Ally Saidi Mwishehe iliibiwa wakati wa wiki, na wanachama walimpa pole kwa sababu ni hasara kubwa kwake. Tuliongea kuhusu umuhimu wa kufuli na kwa waangalifu.

Husein Hamza alisema aliona mpanda baiskeli aliyepata ajali na alijaribu kupiga simu namba za simu tulizopewa na traffic police kwenye kijibatu lakini hazipokelewi hata moja. Tulikubali kuwaambia traffic police kuhusu hiyo.